KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 12, Issue 1
29th RAJAB 1432
1st July, 2011

YALIYOMO

KUSHEREHEKEA SHA'BAAN 1 - 4
NDOA ZA HALALI 4

Kusherehekea "Laylat an-Nisf min Sha'baan"

Samaahat ash-Shaykh 'Abdul-'Azeez ibn Baaz (رحمه الله)

Kila aina ya Shukrani ni zenye kumthubutukia Allaah, ambaye aliyetutakasia Dini yetu, na akatukamilishia fadhla Zake juu yetu. Na Baraka na amani zimshukie Mtume Wake na Mjumbe Muhammad, mtume wa kutubia na Rehma.

Amesema Allaah (kwa maana ya tafsiri): *"This day, I have perfected your religion for you, completed My Favour upon you, and have chosen for you Islam as your religion [al-Maa'idah 5:3]*

"Or have they partners with Allaah (false gods) who have instituted for them a religion which Allaah has not ordained? [al-Shooraa 42:21]

Imepokewa katika swaheeh mbili kutoka kwa 'Aa'ishah (رضي الله عنها) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Yoyote mwenye kuzua kitu katika jambo letu hili [Uislamu] kisichokuwa katika sehemu yake, atakataliwa nacho."

Katika swaheeh Muslim imepokewa kutoka kwa Jaabir (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na mazoeya ya kusema katika khutbah zake za ljumaa: "Maneno yaliyo bora zaidi ni Kitaab cha Allaah na Uongofu ulio bora zaidi ni uongofu wa Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Miongoni mwa yaliyo maovu mno ni mambo ya kuzuliwa, na kila Jambo ovu mno ni la kuzuliwa, na kila jambo la kuzua (bid'ah) ni upotofu." Na kuna Aayaat nyingi sana na ahaadeeth zenye kusema mambo kama hayo.

Hili linaashiriya waziwazi yakwamba Allaah Ameitakasa dini ya Ummah huu, na akakamilisha fadhla Zake juu yao. Hakuuchukuwa uhai wa Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) mpaka alipoufikiliza ujumbe wake kikamilifu na kuufafanulia Ummah kila kitu ambacho alichowafaradhishia Allaah katika maneno na vitendo. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alibainisha yakwamba kila kitakachozuliwa na watu baada ya kufa kwake, maneno yote na vitendo vyote ambavyo watakavyovinasibisha na Uislamu, yote hayo ataregeshewa na kuvurumiziwa Yule aliyeyazua hayo, hata kama niya yake ilikuwa ni nzuri namna gani.

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

قافلة الرحمة للحج والعمرة Al-Rahma `Umrah & Hajj

Agencies1432 Hijri / 2011 C.E

Assalaamu `Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah Safari yetu ya mwaka huu 1432 Hijri/2011 ya kupeleka watu `Umrah katika mwezi wa Ramadhaan, kumi la mwisho. Na vilevile katika `Ibaadah ya Hijjah.

Mipangilio ya Safari ya `Umrah (Mwezi wa Ramadhaan) ni kama ifuatayo:

• Kuondoka ni tarehe 17 ya mwezi wa Ramadhaan*Kurudi ni baada ya `Eid Insha Allaah

• Safari itaanzia Nairobi – Jeddah

• Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli na Usafiri) ni $1500 U.S

• Siku tatu tutakuwa Madinah na Siku kumi za mwisho tutakuwa Makkah mpaka `Eid.

• Safari ya Kurudi Jeddah – Nairobi. Itakuwa baada ya `Eid

Twapenda kuwahimiza wale wale wenye niya ya kwenda na sisi waharakishe kuleta Passport zao na picha Nne kwa ajili ya kufanya maandalizi. Sababu ni kwamba Viza zitafungwa kabla ya mweizi wa Ramadhaan kuanza.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa njia zifuatazo:

• Tutumie e-mail katika info@qssea.net au

• Simu nambari +254 723471820 (Abu Bilaal Athman Na'man)

• Simu nambari +254 721473181 (Abu Farida Muhammad Basawad)

• Simu nambari +254 700365253 (Muhammad Abdillaah)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) waliyajua mas'ala hayo, kama ambavyo wanavyuoni wa Uislamu walivyoyajua baada yao. Waliishutumu bid'ah na wakaonya dhidi yake, kama ilivyonukuliwa na wote wale walioandika vitabu katika kuisifu Sunnah na kuikosoa bid'ah, kama vile Ibn Waddaah, at-Tartooshi, Ibn Shaamah na wengineo.

Miongoni mwa bid'ah zilizozuliwa na baadhi ya watu ni kusherehekea katikati ya mwezi wa Sha'baan (*Laylat an-Nisf min Sha'baan*), na kuifanya siku hiyo makhsusi iwe ni ya kufunga. Hakuna dalili yoyote ya jambo hilo iwezayo kuzingatiwa kuwa ni yenye kutegemewa. Baadhi ya ahaadeeth zilizo dha'eef zimepokewa kuhusu fadhla zake, lakini sisi hatuwezi kuzikubali kuwa ni za kutegemewa. Riwaya zote ambazo zilizopokewa kuhusu fadhla za swala katika tukio hili ni *mawdhoo' (za kuzua*), kama zilivyodondolewa na wanavyuoni wengi. Tutayanukuu baadhi ya maneno yao hapa chini Insha-Allaah.

Vilevile baadhi ya riwaya zimepokelewa kuhusiana na mas'ala haya kutoka kwa baadhi ya Salaf waloko Syria, na sehemu nyenginezo. Wanayoyasema wengi miongoni mwa wanavyuoni ni kwamba kulisherehekea tukio hili ni bid'ah, na kwamba ahaadeeth zote zenye kuhusiana na fadhla za tukio hili ni *dha'eef* na baadhi yake ni *mawdhoo'*. Miongoni mwa walioyasema hayo ni al-Haafidh Ibn Rajab, katika kitabu chake *Lataa'if al-Ma'aarif*, na vyenginevyo. Ahaadeeth zilizo dha'eef zinazohusiana na vitendo vya 'Ibaada zinaweza kutekelezwa katika hali ya vitendo vya 'Ibaada vilivyothibitishwa na dalili zilizo swaheeh. Hapana msingi ulio swaheeh wa kusherehekea katikati ya Sha'baan, kwahivyo hata hapo pia hatuwezi kufuata ahaadeeth zilizo dha'eef.

Msingi huu ulio muhimu mno umetajwa na Imaam Abul-'Abbaas Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله). Wanavyuoni (رحمهم الله) wamekubaliana yakwamba ni waajib kuregesha mas'ala ambayo watu hukhitilafiana kwayo kwenye Kitaab cha Allaah na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Hukmu yoyote watakayoitoa wote au mmojawapo ndiyo Sharee'ah ambayo ni lazima ifuatwe, na lolote lenye kwenda kinyume chake ni lazima likataliwe kabisa. Kwahivyo, vitendo vyovyote vya 'Ibaada ambavyo havikutajwa ndani yake ni bid'ah na hairuhusiwi kuvifanya, licha ya kuwalingania watu au kuwahalalishia wayafanye. Kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى) (kwa maana ya tafsiri): "*O you who believe! Obey Allaah and obey the Messenger (Muhammad), and those of you (Muslims) who are in authority. (And) if you differ in anything amongst yourselves, refer it to Allaah and His Messenger, if you believe in Allaah and in the Last Day. That is better and more suitable for final determination [al-Nisaa' 4:59]*

"And in whatsoever you differ, the decision thereof is with Allaah (He is the ruling Judge)" [al-Shooraa 42:10]

"Say (O Muhammad to mankind): "If you (really) love Allaah, then follow me (i.e. accept Islamic Monotheism, follow the Qur'aan and the Sunnah), Allaah will love you and forgive you your sins [Aal 'Imraan 3:31]

"But no, by your Lord, they can have no Faith, until they make you (O Muhammad) judge in all disputes between them, and find in themselves no resistance against your decisions, and accept (them) with full submission" [al-Nisaa' 4:65]

Na kuna Aayaat nyingi kama hizo zenye kueleza waziwazi yakwamba mas'ala yenye ikhtilafu yanarudishwa kwenye Qur'an na Sunnah, na kwamba hukmu zake hazina budi kukubaliwa. Hili ni sharuti la Imaan na hili ndilo lililo bora kwa watu katika ulimwengu huu na utakaofuata: "*That is better and more suitable for final determination*" *[al-Nisaa' 4:59* – (kwa maana ya tafsiri): katika siku ya Qiyama.

Al-Haafiz Ibn Rajab (رحمه الله) amesema katika kitabu chake *Lataa'if al-Ma'aarif* kuhusu mas'ala haya baada ya kutangulia kuyajadili - "*Laylat an-Nisf min Sha'baan* (katikati yaSha'baan) ilitukuzwa na *ma-Taabi'een* miongoni mwa watu wa Shaam, kama vile Khaalid ibn Mi'daan, Mak-hool, Luqmaan ibn 'Aamir na wengineo, waliokuwa wakifanya juhudi kubwa katika 'Ibaada kwenye usiku huu. Watu wakachukuwa fikra ya fadhla za usiku huu na ya kuitukuza kutoka kwao. Ilisemekana yakwamba wao walisikiya riwaya za *Israiliyyaat* (riwaya za kutoka kwenye asli za Kiyahudi) kuhusiana na hayo. Idadi kubwa ya wanavyuoni kutoka katika sehemu za Hijaaz wameyashutumu hayo wakiwemo 'Ataa' na Ibn Abi Maleekah. 'Abd al-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam alipokea rai hiyo kutoka kwa *ma-fuqahaa*' wa Madeenah, na hii ndiyo rai ya wafuasi wa Maalik na wengineo. Wao wamesema: Hii yote ni bid'ah … Hakuna lililopokewa kutoka kwa Imaam Ahmad kuhusu *Laylat an-Nisf min Sha'baan* … Kuhusu kukesha kwa kuswali katika usiku huo wa katikati ya Sha'baan, hakuna riwaya iliyo swaheeh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au kutoka kwa Maswahaba zake …".

Haya ndiyo yaliyosemwa na al-Haafidh Ibn Rajab (رحمه الله). Alisema waziwazi yakwamba hakuna riawaya iliyo swaheeh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au kutoka kwa Maswahaba zake (رحمهم الله) kuhusu *Laylat an-Nisf min Sha'baan* (katikati ya Sha'baan).

Katika kila hali ikosekanapo dalili ya kisheriya iliyo swaheeh yakwamba jambo Fulani limefaradhishwa katika Uislamu, hairuhusiwi kwa Muislamu kuzua mambo katika Dini ya Allaah,

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

emma mambo haya yatakuwa ni matendo ya ki-binafsi au matendo ya vikundi mbalimbali, emma atayafanya kwa siri au dhahiri, kwa sababu ya maana ya ki-Ujumla ya hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yoyote mwenye kuzua kitu katika jambo letu hili [Uislamu] kisichokuwa katika sehemu yake, atakataliwa nacho." Na kuna dalili (ushahidi) nyengine zenye kuashiriya yakwamba bid'ah ikataliwe na watu waonywe dhidi yake.

Amesema Imaam Abu Bakr al-Tartooshi (رحمه الله), katika kitabu chake *al-Hawaadith wa'l-Bida'*: "Ibn Waddaah alipokea kutoka kwa Zayd ibn Aslam amesema: Hatukuwahi kukutana na yoyote miongoni mwa ma-Shekhe wetu na ma-fuqahaa' walioshughulika na Laylat an-Nisf min Sha'baan, au aliyeshughulika na hadeeth ya Mak-hool, au aliyefikiri yakwamba usiku huu ulikuwa na umuhimu zaidi kuliko usiku mwengine wowote. Ibn Abee Maleekah aliambiwa yakwamba Zayd an-Numayree alisema yakwamba, malipo (thawabu za) ya Laylat an-Nisf min Sha'baan ni kama malipo ya Laylat al-Qadr. Akasema, Iau kama ningelimsikiya akisema hivyo na nikawa nina fimbo mkononi mwangu ningelimchapa. Akasema: "Ziyaad ni mtu wa hekaya."

Al-'Allaamah al-Shawkaani (رحمه الله) amesema katika *al-Fawaa'id al-Majmoo'ah*: "Hadeeth isemayo, 'Ewe 'Ali, yoyote mwenye kuswali rakaa'ah mia moja katika siku ya *Laylat an-Nisf min Sha'baan*, na akasoma katika kila rakaa'ah Surat al-Faatihah na *Qul Huwallaahu Ahad* mara kumi, Allaah atamtakabalia mahitaji yake yote …' Hii ni mawdhoo' (ya kuzua) [yaani; Ni hadeeth ya urongo iliyonasibishwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم)] Matamshi yake yanadhihirisha wazi malipo atakayojipatia mtu mwenye kufanya hayo, na hapana mtu mwenye fahamu zake nzuri awezae kutia shaka yakwamba hii ni hadeeth ya kuzua. Vilevile watu wa isnaad yake ni *majhool* (wasojulikana). Pia imepokewa kwa njia nyengine ya isnaad, ambayo yote ni mawdhoo' (ya kuzua) na wapokezi wake wote ni majhool (wasojulikana). Katika al-Mukhtasar amesema: "Hadeeth kuhusu swala ya katikati ya Sha'baan ni ya urongo, na hadeeth ya 'Ali iliyopokewa na Ibn Hibbaan - "Ifikapo usiku wa katikati ya Sha'baan, jishughulisheni na usiku huo kwa swala na mufunge mchana wake." ni dha'eef. Katika *al-La'aali'* amesema, "Rakaa'ah mia moja ifikapo katikati ya Sha'baan, kusoma Surat al-Ikhlaas mara kumi katika kila rakaa'ah… (Hii ni) *mawdhoo'* (ya kuzua). Na wapokezi wake wote katika isnaad zake tatu ni watu majhool (wasojulikana) na dha'eef". Akasema: "Na rakaa'ah kumi na mbili, usome ikhlaas mara thalathini na tatu katika kila rakaa'ah, hii ni mawdhoo', na rakaa'ah kumi na Nne, hii ni mawdhoo'. Pote la *ma-fuqahaa'* lilihadaiwa kwa hadeeth hii, kama vile mtunzi wa al-Ihyaa' na wengineo, kama walivyohadaiwa pia baadhi ya *mufassireen*.

Swala ya usiku huu - katikati ya Sha'baan ilielezwa kwa njia tafauti, ambazo zote ni dha'eef na zilizozuliwa." Amesema al-Haafidh al-Iraaq: "Hadeeth kuhusu swala katika usiku wa katikati ya Sha'baan imezuliwa na kunasibishwa kwa njia ya urongo na Mtume (صلى الله عليه وسلم)." Imaam an-Nawawee amesema katika kitabu chake *al-Majmoo'*: "Swala iitwayo *Swalaat ar-Raghaa'ib*, ambayo ni rakaa'ah kumi na mbili baina ya Maghrib na 'Ishaa' katika usiku wa Ijumaa ya kwanza katika mwezi wa Rajab, na swala ya *Laylat an-Nisf min Sha'baan,* ya rakaa'ah mia moja - swala hizi mbili ni bid'ah ya kulaumika. Mtu yoyote asidanganyike kwa ukweli yakwamba hayo yametajwa katika vitabu *Qoot al-Quloob na Ihyaa' 'Uloom al-Deen*, au kwa hadeeth iliyotajwa kwenye vitabu hivyo viwili. Yote hayo ni ya urongo. Wala wasidanganyike na ukweli yakwamba baadhi ya ma-Imaam walitatizika kuhusu suala hili na kuandika kurasa chache kueleza yakwamba swala hizi ni mustahabb, kwani wao walikosea hapo."

Shaykh al-Imaam Abu Muhammad 'Abd al-Rahmaan ibn Ismaa'eel al-Maqdisi aliandika kitabu chenye manufaa kuthibitisha yakwamba (riwaya) hizi ni za urongo na akafanya kazi nzuri sana. Wanavyuoni walizungumzia kwa urefu kuhusu mas'ala haya, na Iau kama sisi ingelikuwa tuyanukuu yote hayo tuliyoyasoma kuhusu waliyoyasema kuhusu suala hili, itachukuwa muda mrefu mno. Pengine yale ambayo tuliyoyataja yanatosha kumridhisha mwenye kutafuta ukweli. Kutoka katika aayah za Qur'an, ahaadeeth, na rai za wanavyuoni zilizonukuliwa hapo juu, imemdhihirikia mwenye kutafuta ukweli yakwamba kusherehekea katikati ya Sha'baan kwa kuswali katika usiku huo au kwa njia yoyote, au kwa kuiweka siku hiyo kwa kufunga, ni bid'ah iliyokemewa na wanavyuoni wengi. Haina msingi wowote katika Sharee'ah iliyotwahirika, bali ni mojawapo ya mambo yaliyozuliwa katika Uislamu baada ya zama za Maswahaba (رضي الله عنهم).

Inatosha kwa mwenye kutafuta ukweli , katika hali hii na nyenginezo, kuyajua maneno ya Allaah (kwa maana ya tafsiri): *"This day, I have perfected your religion for you…"[al-Maa'idah 5:3]* na aayaat nyengine zinazofanana na hiyo na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yoyote mwenye kuzua kitu katika jambo letu hili [Uislamu] kisichokuwa katika sehemu yake, atakataliwa nacho." na ahaadeeth nyengine mfano wake.

Katika swaheeh Muslim imepokewa yakwamba Abu Hurairah (رضي الله عنه) amesema: "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Musiutenge usiku maalum wa Ijumaa kwa kuswali qiyaam, na musiitenge siku maalum ya Ijumaa kwa

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

kufunga, isipokuwa ikiwa ni katika kawaida za mmoja wenu katika kufunga."

Lau kama ingelikuwa inaruhusiwa kuutenga usiku wowote kwa ibaadah yoyote maalum, basi usiku wa ljumaa ungelikuwa ndio bora, kwa sababu siku ya ljumaa ndiyo siku bora miongoni mwa masiku jua linapochomoza, kama ilivyonukuliwa katika hadeeth iliyo swaheeh iliyopokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwa vile Mtume (صلى الله عليه وسلم)alitutahadharisha katika kuuchagua usiku huo kwa kuswali qiyaam, hiyo yaashiriya yakwamba imekatazwa zaidi kuuchagua usiku mwengine wowote kwa matendo ya 'Ibaadah, isipokuwa itakapokuwepo dalili iliyo swaheeh kuashiriya yakwamba usiku maalum na uchaguliwe. Kwa sababu imefaradhishwa kujishughulisha kwa 'Ibaadah katika usiku wa Laylatul-Qadr na usiku mwengine wa Ramadhaan kwa ajili ya kuswali. Mtume (صلى الله عليه وسلم)aliwatanabahisha watu kuhusiana na hilo na akawahimiza Ummah wake kuswali qiyaam katika usiku huo (wa Ramadhaan). Yeye mwenyewe pia alilifanya hilo kama ilivyokuja katika swaheehayn, ambapo iliposema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Yoyote mwenye kuswali qiyaam katika mwezi wa Ramadhaan kwa lmaan na kutarajia malipo, Allaah atamsamehe madhambi yake yaliyopita." na "Yoyote atakaejishughulisha na kuswali katika usiku wa Laylatul-Qadr kwa lmaan na kutarajia malipo, Allaah atamsamehe madhambi yake yaliyopita."

Lakini lau kama ingelikuwa imefaradhishwa kuuchagua usiku wa katikati ya Sha'baan, au usiku wa ljumaa ya kwanza katika mwezi wa Rajab, au usiku wa al-Israa' na Mi'raaj, kwa sherehe au kwa maadhimisho yoyote ya 'Ibaadah, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) angeliufundisha Ummah wake kufanya hivyo, na angelilifanya hilo yeye mwenyewe. Lau kama sampuli yoyote (ya 'Ibaadah kama hizo) ingelitokea, basi Maswahaba zake (رضي الله عنهم) wangeliyasambaza kwa Ummah mzima, hawangeliwafichia hayo, kwani wao ndiwo waliokuwa wabora wa watu na wenye *ikhlaas* zaidi, baada ya Mitume (عليهم الصلاة والسلام), na twamuomba Allaah awe radhi na Maswahaba wote wa Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Sasa imeshatudhihirikia kutokana na maneno ya wanavyuoni yaliyonukuliwa hapo juu yakwamba hakuna riwaya kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au kutoka kwa Maswahaba zake (رضي الله عنهم) kuhusiana na fadhla za usiku wa kwanza za ljumaa katika mwezi wa Rajab, au usiku wa katikati ya Sha'baan. Kwahivyo twajua sasa yakwamba kusherehekea matukio haya ni uzushi uliozuliwa kwenye Uislamu, na kwamba kuchagua siku maalum kwa matukio hayo kwa kufanya 'Ibaadah ni bid'ah yenye kulaumiwa. Vilevile utahusika usiku wa tarehe ishirini na saba wa mwezi wa Rajab, ambao baadhi ya watu wanaamini yakwamba ni usiku wa Israa' na Mi'raaj; hairuhusiwi kuichagua tarehe hii kwa matendo ya 'Ibaadah, au kusherehekea tukio hili kutokana na dalili zilizobainisha hapo awali. Hii ni katika hali ambapo iwapo tarehe halisi [ya Israa' na Mi'raaj] inajulikana, sasa huwaje katika ukweli ambapo rai iliyo swaheeh ya wanavyuoni ni kwamba tarehe yenyewe haijulikani! Rai yakwamba ni usiku wa tarehe ishirini na saba katika mwezi wa Rajab ni rai ya makosa ambayo isokuwa na msingi katika ahaadeeth swaheeh. Kwa hakika alisema kweli, yule aliyesema: "Mambo yaliyo bora ni yale yenye kufuata njia za uongofu za salaf, na mambo maovu zaidi ni yale yenye kuzuliwa."

Twamuomba Allaah atusaidie sisi na Waislamu wote katika kushikamana na Sunnah na kujitahadhari na kila kitu chenye kwenda kinyume chake, kwani Yeye Ndiye Mwenye huruma zaidi, na Mkarimu zaidi. Twamuomba Allaah ambariki Mja wake na Mtume, Mtume wetu Muhammad na Ahli zake wote na Maswahaba.

NDOA ZA HALALI

Tukio geni limekuwa la kawaida katika Ummah wa Kiislamu. Na khususan kwa nchi au watu fulani, na matokeo yake yanaletwa na Waislamu wenyewe, yana hatari ya kuleta maafa makubwa kwa jamii ya Kiislamu. Jambo hili ni tisho kubwa kwa idadi ya Waiislamu ambao hawajafunga ndoa. Katika daraja ya ubinafsi, yaweza ikaonekana kuwa upweke unaathiri hatari ndogo mno kwa ummah. Lakini katika Uislamu, kinyume na dini nyingine, mambo hupimwa kulingana na faida zake na madhara yake kwa ujumla. Kwahivyo ni ipi athari ya waliopweke (ukapera) katika jamii? Kulipata jibu, mtu anafaa aangalie jamii zisizo za Kiislamu. Kila siku twakabiliwa na njia za uchafu na uzinifu ambazo *makufaar* wazikubali katika jamii zao. Haya hutokea kwa sababu ya uamuzi wao wa kutofunga ndoa kinyume na *fitrah*. Hakuna Muislamu aliye na akili timamu ambaye atataka ummah huu uanguke katika mila na desturi za kaumu zilizopita za "Pompeii" au "Sodo" na "Gomorrah"- miji ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) aliyoiangamiza kwa sababu ya upotofu, uzinifu na U'asi wao kwa ujumla. Kujilinda na janga kama hilo ni lazima tuwe na ndoa za halali.

JIPATIE NAKALA YA KITABU CHA SWALA:

NAMBARI ZA SIMU NI:

0721473181 AU 0727341779